


# Ufasiri wa Watoto Wasomaji wa Mhusika Aliye na Ulemavu katika Hadithi Teule za Watoto

*Mwendwa, S.M.[1], Ngugi, P.M.Y N.[2], na Mutugu, B.N.[3]*

## IKISIRI

*Makala hii inaangazia namna watoto wasomaji wanavyofasiri mhusika mtoto aliye na ulemavu katika hadithi teule. Katika tasnia ya fasihi kwa jumla, tafiti zinazohusiana na masuala ya ulemavu zimefanywa na watu wengi. Hata hivyo, tafiti nyingi za awali zimeshughulikia mtindo, wahusika, msigano wa majina ya ulemavu na hata semi na lugha. Aidha, katika fasihi ya watoto, tafiti za awali zimelenga mitazamo ya watoto kwa wenzao walio na ulemavu wa kimwili pekee. Ni katika msingi huu ambapo makala hii imeshughulikia namna watoto wasomaji wanavyofasiri mhusika mtoto aliye na ulemavu katika hadithi teule. Ili kufikia azma hii, mtafiti aliwahoji wanafunzi wa gredi ya kwanza na ya pili kutoka shule za msingi Kaunti ya Kiambu. Makala hii imeongozwa na nadharia ya Udenguzi ya Derrida (1976). Kulingana na nadharia hii, matini ya kifasihi inaweza kufasiriwa kwa zaidi ya njia moja. Data iliyochanganuliwa ilikusanywa maktabani na nyanjani. Maktabani mtafiti alisoma machapisho mbalimbali kama vile makala, tasnifu na vitabu. Nyanjani mtafiti aliwasaili wanafunzi wa gredi ya kwanza na ya pili kutoka shule za msingi Kaunti ya Kiambu. Matokeo ya utafiti yalidhihirisha kuwa watoto watafitiwa walifasiri mhusika aliye na ulemavu kwa njia mbalimbali. Kwa mfano, walimfasiri mhusika aliye na ulemavu kama mhusika wa kuendeleza ushirikiano na mapenzi, mwenye uwezo, mwenye kuonewa huruma/ kudunishwa, anayebaguliwa, shujaa, wa kuigwa, anayenyanyapaliwa, wa kudharauliwa na hata mnyonge.*


# 1.0 Utangulizi

Kulingana na sheria za nchi ya Kenya kifungu kinachoshughulikia dhuluma za kijinsia, mtoto anaelezwa kama binadamu au mtu mwenye umri wa miaka kumi na saba kurudi chini (Republic of Kenya, 2006). Kwa mujibu wa Shirika la Kazi Duniani (2007) mtoto ni mtu aliye na miaka chini ya kumi na minane. Hata hivyo, Bakize (2014) ameieleza dhana ya mtoto kwa kurejelea; jamii, utamaduni na dini. Kwa kuzingatia jamii na tamaduni anaeleza kuwa, umri na ukuaji ndio unaotumika kumtofautisha mtoto na mtu mzima. Aidha, kwa kurejelea dini mbalimbali, Bakize anasema kuwa, binadamu wote ni watoto mbele ya Mwenyezi Mungu. Ni wazi kwamba, fasili ya mtoto ina utata kuieleza. Katika utafiti huu tumechukulia mtoto kama binadamu aliye kati ya miaka sita hadi saba. Kulingana na Ngugi (2013) fasihi ya watoto huandikwa ili kumlenga msomaji ambaye uzoefu wake wa maisha sio mpana na uelewa wake wa mambo ungali unaendelea kukua. Kwa hivyo, dhamira ya fasihi hii ni kuwahusisha watoto ambao wanakua kimaumbile, kiakili na kilugha.

Dhana ya ulemavu imefasiliwa na watalamu mbalimbali (Howard, 1999; NCPWD, 2003, Shirika la Kazi Duniani, 2007, Republic of Kenya, 2010, Mahenge, 2017, Mutugu, 2019). Kwa mfano; Howard (1999) anasema kwamba, watu wenye ulemavu ni kikundi cha watu wasiojiweza na ambao wametengwa zaidi katika jamii. Kwa mujibu wa kifungu cha sheria cha NCPWD (2003) na Katiba ya Kenya (2010); ulemavu unaweza ukawa wa kimwili, kihisia, kiakili au ugonjwa ambao athari zake ni za muda mrefu na hivyo basi kumzuia mtu kutekeleza shughuli zake za kawaida za kila siku. Shirika la Kazi Duniani (2007) wameeleza ulemavu kama hali ya kukosa kiungo cha kutekeleza shughuli za kawaida za kila siku kama watu wengine. Kwa mujibu wa Mahenge (2017) watu wenye mahitaji maalumu au walemavu ni kama vile; walemavu wa viungo, albino, viziwi, wasioona, bubu, viziwiwasioona, viziwibubu na viziwiwasioonabubu. Naye, Mutugu (2019) anaeleza kuwa, ulemavu ni hali inayoonesha kupungukiwa kwa namna fulani kwa mtu kutokana na namna anavyoonekana na hata tabia zake. Kutokana na fasili hizi, mlemavu ni binadamu aliye na hitilafu za kimaumbile za kudumu.

## 2.0 Msingi wa Nadharia

Makala hii imeongozwa na nadharia ya Udenguzi iliyoasisiwa na Jacques Derrida mnamo mwaka wa 1976. Aidha, nadharia hii imeendelezwa na waitifaki kama vile; Wafula na Njogu (2007), Sikirivwa (2015), Omoga, (2018) mingoni mwa wengine. Kwa mujibu wa nadharia hii, matini ya kifasihi inaweza kufasiriwa kwa zaidi ya njia moja. Hivyo basi, nadharia ya Udenguzi ilimfaa mtafiti kushughulikia namna watoto wasomaji wanavyofasiri mtoto aliye na ulemavu kama mhusika katika hadithi teule. Hasa mhimili unaosema kwamba, hakuna kazi ya mwisho ya kifasihi. Kulingana na mhimili huu fasiri mbalimbali zinaweza kutolewa na wahakiki tofauti kuhusu jambo moja ambalo huweza kukinzana maadamu wana ushahidi wa kutosha.

## 3.0 Mbinu za Utafiti

Mtafiti aliwaongoza watoto wa gredi ya kwanza katika usomaji wa hadithi ya *Rafiki yangu Kilomi* (Rajula, 2019) na *Tupendane Sote* (Maina, 2022). Vilevile, aliwaongoza watoto wa gredi ya pili katika usomaji wa hadithi ya *Daudi Mlemavu* (Jefwa, 2000) na *Kesho! Kesho!* (Hus - sein, 2009). Hadithi teule ziliteuliwa kimakusudi. Kulingana na Kombo na Tromp (2006) uteuzi wa kimakusudi wa data unahusu uteuzi wa moja kwa moja wa data yenye sifa zinazolengwa na utafiti husika. Aidha, baada ya watoto watafitiwa kusoma, mtafiti alitumia kielelezo cha maswali kuwauliza watoto swali na kisha kuwarekodi wakijibu swali lengwa. Mtafiti alisikiliza majibu ya watafitiwa kutoka aina tatu za kanda na kisha kunakili na kuchambua ufasiri wao kuhusu namna wanavyofasiri mhusika aliye na ulemavu. Isitoshe, maadili ya kitafiti yalizingatiwa wakati wa utafiti.

## 4.0 Dhana ya Ufasiri

Kwa mujibu wa Levinson na Mailloux (1988) ufasiri ni hali ya kuunda au kueleza maana tofauti baada ya usomaji. Sumara (2002) anasema kwamba, ili upate uelewa wa kitu, unahitaji kukifasiri. Taylor (2014) anaongeza kwamba, ufasiri katika fasihi ni kufafanua au kutoa maana ya maneno katika muktadha wake. Mpemba (2015) anaeleza kwamba, ufasiri ni hali ya kutoa maoni yako mwenyewe baada ya kusikiliza yaliyosemwa au kuandikwa na mtu mwingine. Aidha, kulingana na https://www.vocabulary.com, ufasiri ni kitendo cha kueleza, kuunda upya, au vinginevyo kuonesha uelewa wako wa jambo fulani. Kutokana na fasili zilizotolewa na wataalamu hawa, ni wazi kwamba, ufasiri ni kueleza kitu au kukitolea maoni kulingana na uelewa wa mtu binafsi. Dhana hii ya ufasiri ni muhimu katika makala hii kwani imezingatiwa katika kazi za watoto zilizo na wahusika walio na ulemavu.

### 4.1 Ufasiri wa Mhusika Mtoto Mlemavu kulingana na Wanafunzi wa Gredi ya Kwanza

Mtafiti aliwaongoza wanafunzi teule wa gredi ya kwanza kueleza ufasiri wao kuhusu mhusika mtoto aliye na ulemavu baada ya kusoma hadithi ya *Rafiki yangu Kilomi* (2019) na *Tupendane Sote* (2022). Baada ya kusoma hadithi teule watafitiwa walifasiri mhusika aliye na ulemavu kama mwenye kuendeleza ushirikiano na mapenzi, mwenye uwezo, mwenye kuonewa huruma/ kudunishwa na hata anayebaguliwa.

#### 4.1.1 Mlemavu kama Mhusika Mwenye Kuendeleza Ushirikiano na Mapenzi

Kwa mujibu wa BAKIZA (2010) mapenzi ni hisia nzito ya moyoni inayomfanya mtu avutiwe, athamini na ajali mtu, kitu au jambo fulani. Isitoshe, Ali (2019) anaongeza kuwa, mapenzi ya urafiki yanahusu kutendeana wema, hayana uchu au hamu ya kingono. Mapenzi huhusisha uaminifu kwa familia, jamii na marafiki.

Dhamira kuu ya hadithi ya *Tupendane Sote* (2022) ni kupenda watu bila ya kujali maumbile yao. Katika hadithi ya *Tupendane Sote* (2022), jamii ya msimulizi inasawiriwa kama iliyo na chuki kwa mhusika mtoto mlemavu lakini mwishowe, inaishia kumpenda baada ya kuona namna anavyowashirikisha wenzake na hata kuwapenda. Mathalan, mwanzoni mwa hadithi, watoto wasio na ulemavu walimtenga mhusika Eli na hawakutaka kushirikiana naye. Zaidi ya hayo, watoto waliohusishwa katika utafiti wana eleza kuwa mhusika mlemavu anastahili kushirikishwa katika shughuli zote na hata kupendwa kutoka mwanzo wa hadithi hadi mwisho. Kwa mfano, baadhi ya wanafunzi walitoa maoni yao kama ifuatavyo:

**SJ[1]:** Tuwe marafiki kama alivyofanya Eli. Tucheze pamoja kama alivyofanya Eli.

**SJ:** Tupendane sote kama mhusika Eli alivyowapenda wenzake.Tusipigane kwa sababu ya mpira, tuige Eli.

**SU:** Tusaidiane sisi sote bila kujali maumbile kama vile Eli.Tusiumizane hisia zetu, tuwe kama Eli.

Kauli za watoto kutoka SK, SJ na SU zinaashiria kwamba, mhusika aliye na ulemavu amesawiriwa kama mwenye kuendeleza ushirikiano na mapenzi. Isitoshe, wanafunzi wa SK waliongeza kuwa, mhusika mtoto aliye na ulemavu ana mapenzi mengi kwani aliwasaidia wenzake kutoa mpira uliokwama kwenye ua. Aidha, watoto kutoka SJ walisema kwamba, kitendo cha Eli kuwasaidia na hata

kujiunga na wenzake ambao hawakutaka kucheza naye awali, ni thibitisho kuwa, mtoto mhusika mwenye ulemavu ni mwepesi wa kusamehe na mwenye kuonesha ushirikiano na mapenzi. Kulingana na watoto kutoka SU, ni vyema kuthamini na hata kucheza na watoto walio na ulemavu ili kuzuia kuwaumiza nafsi zao. Kauli za watoto wa SU

[1] SK -Shule ya Kawaida, SJ -Shule Jumuishi na SU- Shule ya watoto walio na ulemavu.

inaingiliana na maoni ya Macharia (2021) anayesema kuwa, mapenzi ni msukumo wa ndani ambao humfanya binadamu kumthamini mwengine. Vilevile, wanafunzi hao walikashifu kitendo cha mhusika Ani cha kuchochea wenzake ili kutocheza na Eli.

Katika hadithi ya *Rafiki yangu Kilomi* (2019) suala la mapenzi linajitokeza. Dhamira kuu ya hadithi ya *Rafiki yangu Kilomi* (2019) ni kuonesha mapenzi kati ya marafiki wawili wanaopendana. Maoni ya wanafunzi baada ya kusoma hadithi ya *Rafiki yangu Kilomi* (2019), yalikuwa kama ifuatavyo:

SK: Rafiki yangu.
Kilomi anapenda rafiki yake kwa kuwa, anamsaidia kusukuma kiti chake cha magurudumu.

SJ: Tuwe marafiki kama Kilomi na rafiki yake.

SU: Tusaidie marafiki zetu.
Usichukie mtu aliye na ulemavu kwani watu walio na ulemavu wanapenda watu wengine.
Usiache mtu aliye na ulemavu kwenye barabara, mfanye rafiki yako kama vile Kilomi na rafiki yake.

Kulingana na watoto kutoka SK, SJ na SU mhusika aliye na ulemavu katika hadithi ya *Rafiki yangu Kilomi* (2019) ni mhusika anayee eendeleza mapenzi. Urafiki baina ya Kilomi na rafiki yake unadhihirisha mapenzi kati ya watu wenye ulemavu hadi wale ambao hawana ulemavu. Watoto wa SK, SJ na SU walipendekeza kuwa, watu wanastahili kuwa marafiki na hata kupendana kama vile, Kilomi na rafiki yake bila kujali maumbile. Maoni ya watoto kutoka SK, SJ na SU yanaingilina na mawazo ya Policarpo (2015) anayesema kuwa, urafiki hutokea baina ya watu wawili ambao wanapendana na kusaidiana katika kila hali. Pia, anasisitiza kuwa, mapenzi na usaidizi yanastahili kutoka pande zote. Aidha, watoto kutoka SU waliongeza kuwa,endapo utapatana na mtu ambaye hana mguu, usimchukie. Ni wazi kwamba, watafitiwa wameonesha mapenzi kwa watu walio na ulemavu na huenda ni kwa sababu mhusika mtoto mlemavu amesawiriwa kama mtu mwenye mapenzi.

### 4.1.2 Mlemavu kama Mhusika Mwenye Uwezo

Aidha, watafitiwa walisema kuwa mhusika aliye na ulemavu ni mwenye uwezo. Uwezo ni hali ya kuweza kufanya jambo. Kulingana na wanafunzi waliohusishwa katika utafiti baada ya kusoma hadithi ya Rafiki yangu Kilomi (2019), watafitiwa wa walidai kwamba, mhusika mlemavu ni mtu mwenye uwezo wa kufanya mambo mbalimbali kama vile:

SK:Kuimba.
Kucheka.
Kusoma hadithi.
SJ:Kuketi.
Kuhesabu.
Kupunga mkono.
SU:Kuendesha kiti cha magurudumu kama sisi.
Kuongea na kusikia.
Kusikia na hata kutaniana na wenzake.

Wanafunzi kutoka SK, SJ na SU walieleza uwezo wa mhusika aliye na ulemavu na ufasiri wao ulimsawiri mhusika mwenye ulemavu kama mwenye uwezo wa; kuimba, kucheka, kusoma hadithi, kuketi, kuhesabu, kupunga mkono, kuendesha kiti cha magurudumu, kuongea, kusikia na hata kutaniana na wenzake. Kwa mujibu wa Leininger, Dyches, Prater na Heath (2010) matumizi ya fasihi ya watoto kuhusu watu wenye ulemavu darasani ina madhumuni mawili.

Kwanza, kwa wanafunzi walio na ulemavu, kazi hizi za kifasihi zina mchango mkubwa kwao kwani zinaimarisha utambulisho wao kwa njia chanya. Aidha, kazi za kifasihi zinaweza kuwapa wanafunzi wote maarifa sawia kuhusu watu walio na ulemavu na hivyo basi, kurekebisha dhana potofu zilizozoeleka kama za kawaida. Vilevile, wanafunzi kutoka SU walijinasibisha na mhusika Kilomi katika hadithi ya *Rafiki yangu Kilomi* (2019).

Wanafunzi hao walidai kuwa, mhusika Kilomi alitumia kiti cha magurudumu kama wanavyofanya baadhi yao. Vilevile, waliongeza kuwa, Kilomi anaweza kufanya mazungumzo ya kawaida na rafiki yake. Pia, waliweza kubaini kuwa, mhusika Kilomi ana uwezo wa kuandika, kuvaa nguo na hata kudensi, masuala ambayo hayajatajwa na msimulizi wa hadithi. Kulingana na Beckett, Ellison, Barrett, na Shah (2010) aina ya fasihi ambayo husomwa na watoto, huenda ikaathiri mitazamo yao ya kijumla kuhusu maisha ya wanajamii. Hivyo basi, ni muhimu kwa wandishi kushugulikia mitazamo ya usawa katika masuala ya ulemavu. Isitoshe, kulingana na United Nations (2022), mtu mwenye ulemavu ni binadamu mwenye uwezo na udhaifu sawia na mtu mwingine yeyote. Kauli hizi zinaonekana kuingiliana na maoni ya watoto watafitiwa ambao walikubaliana kwamba, ingawa Kilomi alikuwa na ulemavu wa miguu, alikuwa na uwezo wa kufanya mambo mengine yafanywayo na watu wengine wasio na ulemavu.

Vilevile, uwezo wa mhusika mtoto mlemavu pia ulijadiliwa kupitia mhusika Eli katika hadithi ya Tupendane Sote (2022). Watoto watafitiwa walitoa maoni yao kuhusu ufasiri wao kuhusu watu walio na ulemavu. Walisema kuwa:

SK:Watu walio na ulemavu wana uwezo wa kusaidia watu wengine.

SJ:Watu wenye ulemavu wanaweza kusaidia watu wasio na ulemavu kama vile;

Eli. SU:

Watu wenye ulemavu wanajiweza licha ya ulemavu wao.

Tusidharau watu wenye ulemavu, wanaweza kusaidia.

Watu wenye ulemavu wanaweza kucheza kama wengine ambao hawana ulemavu.

Watoto kutoka SK na SJ walikubaliana kwamba, watu walio na ulemavu wana uwezo wa kusaidia watu wasio na ulemavu. Katika hadithi ya Tupendane Sote (2022), mhusika Eli ana ulemavu wa miguu hata hivyo, anawashangaza wengi kwani anaibuka na suluhu ya matatizo, kitu ambacho wenzake wanashindwa kuwazia. Kwa mfano, Eli anatumia kijiti kuwatolea watoto wenzake mpira ambao ulikuwa umekwama juu ya ua. Tazama Uk. 12 katika hadithi ya Tupendane Sote (2022) ambapo msimulizi anaeleza kwamba:

Eli anachukua ufito mrefu. Anaugonga mpira na kuuangusha. Lino anamwambia wacheze pamoja. (Uk. 12).

Aidha, kulingana na watafitiwa kutoka SU, mtoto aliye na ulemavu ana mchango mkubwa katika jamii kwa mfano, mhusika Eli anapowasaidia wenzake kupata mpira wao uliokuwa umekwama kwenye juu ya ua. Vilevile, waliongeza kwamba, watu walio na ulemavu wana uwezo wa kutekeleza majukumu sawia na watoto wengine ambao hawana ulemavu kama vile; kucheza. Hivyo, walisisitiza kwamba, ulemavu sio kikwazo cha kufanya mambo. Kutokana na mdahalo wa darasani na wanafunzi wa SU, ilibainika kuwa, mtoto mhusika mlemavu amekuzwa na kusawiriwa kama mtu mwenye uwezo wa kuwafaa wengine licha ya maumbile yake tofauti.

### 4.1.3 Mlemavu kama Mhusika Mwenye Kuonewa Huruma/ Kudunishwa

Hata baada ya kudhani kwamba mhusika aliye na ulemavu ni mwenye kuendeleza ushirikiano na mapenzi na hata mwenye uwezo, baadhi ya watoto wengine kutoka SK, SJ na SU walikuwa na maoni hasi kumhusu mhusika aliye na ulemavu. Kwa mfano, katika hadithi ya *Tupendane Sote* (2022) mhusika mkuu Eli amesawiriwa kama kiumbe wa kuonewa huruma kwa kuwa na ulemavu wa miguu. Hili linamfanya aonekane kama kiumbe duni. Duni ni dhana inayoashiria kitu hafifu kilicho na thamani ndogo. Mtafiti alipowauliza watoto kutoa maoni yao kuhusu mhusika Eli baada ya kusoma hadithi ya *Tupendane Sote* (2022), walisema yafuatayo:

SK:Eli ni mnyonge kwani analia.

SJ:Tusaidie wale ambao hawawezi kutembea.

Tusaidie walio na ulemavu.

SU:ucheze na watu walio na ulemavu lakini polepole.

Tucheze na watu walio na ulemavu vizuri.

Maoni ya wanafunzi kutoka SK, SJ na SU yanaashiria kwamba, mhusika aliye na ulemavu amehurumiwa na hata kudunishwa. Kwa mfano, mtafitiwa kutoka SK alidai kuwa, Eli ni kiumbe duni kwani analia bure baada ya wenzake kumbagua baada ya kukataa kucheza naye.

Aidha, watoto kutoka SJ walieleza kwamba, watoto walio na ulemavu wa miguu au aina nyingine ya ulemavu wanahitaji usaidizi ili kutekeleza shughuli zao kwani watoto hao ni viumbe duni. Kulingana na SU, watoto wanapaswa kucheza na watoto wenzao walio na ulemavu japo kwa njia ya polepole. Wanafunzi kutoka SU walikiri kwamba, mhusika mtoto aliye na ulemavu ni kiumbe duni hata hivyo, wenzake wanastahili kumvumilia na hata kucheza naye vizuri na polepole ili kuzuia kumuumiza. Aidha, walisisitiza kuwa, wanafunzi katika jamii ya msimulizi hawakutaka kucheza na Eli kwa kuwa na ulemavu na kukosa nguvu za kucheza mpira kwa kuhofia kumuumiza. Kauli hii inaingiliana na maoni ya Rubin na Watson (1987) wanaoeleza kwamba, watu wenye ulemavu huchukuliwa kama viumbe dhaifu, duni na pia, wasioweza kuwa binadamu kamili kwa sababu, wana kasoro za; kiakili, mwonekano wa kimwili na pia, hawawezi kufanya kazi. Kauli za watoto watafitiwa zinaonesha kwamba, wana uelewa kuwa, watoto walio na ulemavu ni viumbe dhaifu na hawana nguvu kama watoto wengine ambao hawana ulemavu wa mwili.

Mhusika Kilomi katika hadithi ya *Rafiki yangu Kilomi* (2019) ni mvulana aliye na ulemavu wa miguu na hawezi kutembea bila ya kiti chake cha magurudumu. Kilomi anamtegemea rafiki yake kumsukuma ili kufanya shughuli zake za kila siku. Wanafunzi teule walitoa maoni yao kuhusu mhusika Kilomi baada ya kusoma hadithi ya Rafiki yangu Kilomi (2019) na kueleza kwamba, mtoto mhusika mlemavu hawezi:

- SK:Kutembea.
- Kucheza mpira wa kandanda.
- SJ:Kuruka.
- Kukimbia.
- Hawezi kwenda pahali peke yake.

SU:Kusimama na kufanya kazi miongoni mwa shughuli nyingine.
Hawezi kushika kitu kizito.

Kauli hizi kutoka kwa SK, SJ na SU zinaonesha kwamba, mtoto mhusika aliye na ulemavu ni kiumbe duni kwani kuna mambo mengi ambayo hawezi kufanya kama vile; kutembea, kucheza mpira, kuruka, kukimbia, kwenda pahali peke yake, kushika kitu kizito, kusimama, kufanya kazi miongoni mwa shughuli nyingine. Maoni haya ya wanafunzi watafitiwa yanaingiliana na mawazo ya Cameron (2014) ambaye anasisitiza kwamba, mtu mwenye ulemavu huchukuliwa kama binadamu asiye na maana na mzigo kwa jamii kwani hawezi kujitegemea kabisa kwa kila jambo. Wanafunzi kutoka SK, SJ na SU walikubaliana kwamba, mtoto mwenye ulemavu hawezi kufanya mambo mengi kwani ni kiumbe duni na lazima awe na msaidizi. Kadhalika, katika hadithi ya *Rafiki yangu Kilomi* (2019), msimulizi amemtumia mhusika Kilomi kumdunisha mhusika mtoto mlemavu na hivyo basi kumsawiri kama mnyonge au duni. Mnyonge ni mtu asiyekuwa na nguvu na hata wa kuhurumiwa.

### 4.1.4 Mhusika Mlemavu kama Anayebaguliwa

Ubaguzi ni mfumo wa kijamii wa kutoa huduma kwa upendeleo kwa misingi ya rangi, jinsia, kabila au hata maumbile. Kulingana na Dulin-Keita, Hannon Iii, Fernandez na Cockerham (2011) ubaguzi ni suala nyeti linalostahili kushughulikiwa kwani, lina madhara makubwa kwa afya ya kihisia na kiakili kwa watoto. Isitoshe, ubaguzi hautokani na ulemavu wa watoto, bali ni ukosefu wa uelewa kuhusu sababu na athari za ulemavu na pia, mawazo potofu kuhusu ulemavu (UNICEF, 2013). Kwa mujibu wa Tanjung (2020) mtu aliye na ulemavu anaweza kubaguliwa kwa kuwa katika kundi la walio wachache na tofauti katika jamii. Kwa mfano, mhusika Eli, mtoto aliye na ulemavu wa miguu anabaguliwa na wenzake kwa kuwa na maumbile tofauti. Aidha, watoto kutoka SK, SJ na SU walitoa maoni yao kuhusu ubaguzi dhidi ya mhusika mtoto aliye na ulemavu katika hadithi ya *Tupendane Sote* (2022) na kupinga kubaguliwa kwa watoto wenye ulemavu:

SK:Usimdharau mtu kwa kuwa na ulemavu.
Tucheze pamoja.
SJ:Usikatae kucheza na wenzako.
SU:Eli anakaa peke yake kwani anabaguliwa na wenzake.

Kulingana na watoto kutoka SK, si vyema kumdharau mtu aliye na ulemavu kwani kwa kufanya hivyo, atahisi kana kwamba amebaguliwa. Aidha, watoto kutoka SJ walidai kuwa, si vizuri kukataa kucheza na watu walio na maumbile tofauti kama walivyofanya wanafunzi katika jamii ya msimulizi kwa kumbagua mhusika Eli. Kulingana na Tanjung (Keshatajwa), ni vyema kuwaelimisha watoto kuhusu ubaguzi mapema iwezekanavyo ili kuzuia na kupunguza visa vya ubaguzi wa aina yoyote

Isitoshe, watoto kutoka SU walieleza kuwa, mhusika Eli alijitenga na wenzake kutokana na ubaguzi ulioendelezwa na wenzake dhidi yake. Vilevile, wanafunzi kutoka SU waliongeza kuwa, watu walio na ulemavu wanabaguliwa sana hata katika maisha halisia sawia na hadithini. Kauli hii inaungwa mkono na Kristanti (2016) anayesisitiza kwamba, watu walio na ulemavu hubaguliwa katika shughuli za kuchumi, elimu miongoni mwa taaluma nyinginezo. Hii inaonesha kwamba, mhusika aliye na ulemavu anabaguliwa.

Aidha, mawazo ya Derrida (1976) katika nadharia ya Udenguzi yanaingiliana na kauli za wanafunzi kutoka SK, SJ na SU. Derrida (Keshatajwa) anasema kwamba, hakuna kazi ya mwisho ya kifasihi. Fasiri mbalimbali zinaweza kutolewa na wahakiki tofauti kuhusu jambo moja ambalo huweza kukinzana maadamu wana ushahidi wa kutosha. Watafitiwa walitoa maoni mbalimbali kuhusu mhusika aliye na ulemavu kwa mfano, walianza kwa kusema kwamba ni mwenye kuendeleza ushirikiano na mapenzi, mwenye uwezo, mwenye kuonewa huruma/ kudunishwa na hata mwenye kubaguliwa.

## 4.2 Ufasiri wa Mhusika Mlemavu kulingana na Wanafunzi ya Gredi ya Pili

Sehemu hii imeangazia ufasiri wa mhusika aliye na ulemavu kulingana na wanafunzi wa gredi ya pili katika shule teule za msingi, katika Kaunti ya Kiambu. Watoto kutoka SK, SJ na SU walichambua hadithi ya *Daudi Mlemavu* (Jefwa, 2000) na *Kesho! Kesho!* (Hussein, 2009) na kumfasiri mhusika aliye na ulemavu kama; shujaa, wa kuigwa, anayenyanyapaliwa, wa kudharauliwa na mnyonge.

### 4.2.1 Mlemavu kama Mhusika Shujaa

Baada ya kusoma hadithi ya *Daudi Mlemavu* (Jefwa, 2000), watoto kutoka SK, SJ na SU walinasibisha matendo ya Daudi na mtu shujaa. Kulingana na Gichamba (2005) shujaa huwa na tabia ya kushangaza kiasi kwamba, wanajamii humwona kama mtu wa ajabu. Maoni waliyotoa yalionesha ufasiri wao kuhusu mhusika mtoto aliye na ulemavu. Walisema kwamba;

SK:Daudi anaweza kila kitu.

SJ:Tusaidie wenzetu ambao wana shida kama vile Daudi alivyomsaidia mama.

Daudi anapongezwa na mhusika Mama kwa kuwa shujaa.

SU:Daudi ni shujaa kwa kuwa alisaidia mhusika Mama na pia, aliangaziwa katika vyombo vya habari.

Daudi anapongezwa kwa kuwa shujaa na Mwalimu mkuu.

Kulingana na watoto wa SK, SJ na SU, Daudi ana uwezo wa kusaidia wanajamii kwa mfano, wakati wanapokumbwa na changamoto. Kauli hii inaonesha kuwa, watafitiwa hawa waliamini kwamba, licha ya ulemavu, Daudi anaweza kutegemewa na hata kujisaidia yeye mwenye. Watoto kutoka SK, SJ na SU walimwona Daudi kama shujaa baada ya kumkabili na kumshinda mwizi. Maoni ya wanafunzi hawa yanaingiliana na mawazo ya Aylestock (2009) ambaye anasema kuwa, shujaa ni mtu ambaye ana uwezo wa kukabiliana na mhusika mpinzani na kuibuka mshindi. Aidha,wanafunzi kutoka SJ walieleza kuwa, ni vyema kuwasaidia wenzao ambao wanakumbwa na matatizo na wapo katika hali ya hatari. Mathalan, mhusika Daudi alitumia mkongojo wake kumtega mwizi ambaye alikuwa amewakwepa watu wasio na ulemavu na wakashindwa kumshika. Daudi mlemavu alihatarisha maisha yake ili kumnasa mwizi wa kibeti cha mhusika Mama. Kauli za watoto kutoka SJ zinaingilina na maoni ya Mwanzu (2021), anayesema kuwa, shujaa ni binadamu aliye na moyo thabiti na ana uwezo wa kukabili masuala hatari katika jamii. Aidha, watoto wa SJ walieleza kuwa, mhusika Mama alimpongeza Daudi kwa sababu ya ujasiri wake kwa kumpa shilingi elfu moja. Vilevile, watoto wa SU walieleza kuwa, mhusika Daudi ni shujaa kwa vile; aliangaziwa katika vyombo vya habari na wanahabari ambao walitambua juhudi zake za kumnasa mvunja sheria. Kulingana na Pirsl na Popovska (2013), vyombo vya habari ni tasnia muhimu katika maisha ya binadamu hasa katika usambazaji wa habari kwa watu wengi. Kwa hivyo, vyombo vya habari vinaweza kutumika kusambaza habari za kuelimisha kwa wanajamii kuhusu uwezo wa mtu aliye na ulemavu kama vile mhusika Daudi. Lidubwi (2017) anaongeza kwamba, vyombo vya habari vina uwezo wa kuathiri maoni na mitazamo ya umma kuhusu watu wanaoishi na ulemavu kwa njia chanya kama tunavyoona kwa mhusika Daudi.

Aidha, maoni ya watoto kutoka SU yanaingiliana na yale ya Ayala (1999) ambaye anasema kuwa, katika fasihi ya kisasa ya watoto, uwakilishi wa ulemavu mara nyingi huhusishwa na ujasiri. Kwa mfano, katika hadithi ya *Daudi Mlemavu* (2000) msimulizi amemtumia jasiri mhusika Daudi aliye na ulemavu ili kuonesha kwamba, watu walio na ulemavu wanaweza wakawa shujaa. Isitoshe, watoto kutoka SU walieleza kuwa, ushujaa wa Daudi ulishabikiwa na mwalimu mkuu hasa Daudi aliporejea shuleni. Mwalimu mkuu wa shule ya msingi ya Mudete alimuita Daudi mbele ya shule nzima na kumpongeza kwa sababu ya ushujaa wake. Baadaye, msimulizi anamsawiri mhusika Daudi kama shujaa. Mhusika Daudi alibadili msimamo wa kuhama shule ya jumuishi hadi ile ya watoto walio na ulemavu kwa kuwa alitambua kuwa yeye ni shujaa.

### 4.2.2 Mlemavu kama Mhusika wa Kuigwa

Baadhi ya vitabu vya watoto vimewasawiri wahusika wa aina mbalimbali wakiwemo wahusika walio na ulemavu ili kuwasaidia watoto wasomaji kujifunza kuhusu watu walio na ulemavu na hata kuwasaidia walio na ulemavu kuwa na mazoea ya kusoma kwa lengo la kujifurahisha kwa kujinasibisha na wahusika kama wao (Kristanti, 2016). Isitoshe, Azano, Tackett na Sigmon (2017) wanasema kuwa, kusoma na kuchambua kazi za fasihi zinazojumuisha wahusika walio na ulemavu kunaweza kutumika kama njia bora ya kielimu ya kusaidia wanafunzi kujifunza kuhusu watu walio na ulemavu. Kwa mfano, kutokana na maoni ya watoto kutoka SK, SJ na SU hadithi ya *Daudi Mlemavu* (Jefwa, 2000), imemsawiri mhusika aliye na ulemavu kama mtu wa kuigwa. Hizi hapa kauli za watoto waliotafitiwa:

SK:Tusaidie wenzetu ambao wana shida kama vile Daudi alivyomsaidia mama mmoja huko mjini aliyeibiwa kibeti chake na mwizi.

SJ:Daudi anawasamehe waliomdharau.

Watu walio na ulemavu wanaweza kufanya kila kitu.

SU:Tusimchokoze mtu aliye na ulemavu kwani anaweza kusaidia mahali pengine.

Tusamehe wanaotuchekelea kama alivyofanya Daudi.

Kulingana na watafitiwa kutoka SK, mhusika Daudi ni wa kuigwa kwani anamsaidia mama mmoja aliyeibiwa kibeti chake na hivyo basi kuonesha utu. Aidha, watoto kutoka SJ na SU walieleza kuwa, licha ya Daudi kusumbuliwa na hata kudhihakiwa na wenzake kwa kuwa na ulemavu, mhusika Daudi anawasamehe wanafunzi wenzake na hata kubadili nia yake ya kutaka kujiunga na shule ya watoto walio na ulemavu. Daudi anaamua kubakia shule ya watoto jumuishi ya Mudete. Watoto wa SJ na SU vilevile, walisema kuwa ushujaa wa mhusika mwenye ulemavu ni kitu cha kuigwa hasa kipindi kile alichomnasa mwizi. Sifa hizi za Daudi zinamfanya kufasiriwa na watoto kutoka SJ na SU kama mhusika wa kuigwa. Kauli za watoto kutoka SK, SJ na SU zinashahabiana na maoni ya Crow (1990) anayesema kuwa, fasihi ya watoto ina maudhui ambayo yametumika mara kwa mara kumsawiri mtu aliye na ulemavu kama mtu wa kutia watu moyo.

Katika hadithi ya *Kesho! Kesho!* (Hussein, 2009) mhusika Kalpan mtoto aliye na ulemavu wa macho na ambaye alilazimika kuvalia miwani ya kuonea, ni mvulana anayestahili kuigwa. Hii ni kulingana na maoni ya watoto kutoka SK, SJ na SU wanaosema kuwa:

SK: Tuwe marafiki wazuri kama Kalpan.

Usijifananishe na mtu mgonjwa.

SJ:Hatufai kudanganya ili tufanane na wengine.

Hatufai kulilia kila kitu.

SU:Tusijifanye watu walio na ulemavu.

Tuige tabia nzuri za watu na sio mapungufu yao.

Kulingana na watoto kutoka SK, ni vyema kuwa na rafiki mzuri kama Kalpan ambaye anaweza kukuelimisha kuhusu masuala ya ulemavu. Kalpan alimuelimisha rafiki yake Juma kuhusu ulemavu wa macho pamoja na matumizi ya miwani na hivyo basi, ni mhusika wa kuigwa. Maoni ya watoto kutoka SK yanaingiliana na maoni ya Zhang na Morrison (2010) wanaoeleza kuwa, hadithi za watoto zinaweza kutumika kama njia ya kupitisha maadili kwa wanafunzi. Aidha, watoto kutoka SK waliongeza kwamba, si sawa kuiga watu wagonjwa. Watoto kutoka SK, SJ na SU wanakubaliana kwamba, watu hawapaswi kudanganya wala kujifananisha na wenzao walio na ulemavu. Kauli hizi za watoto zilitokana na tabia ya Juma ya kutaka kuiga ulemavu wa macho wa Kalpan ingawa yeye hana ulemavu wa macho. Aidha, watoto kutoka SU walisisitiza kuwa, ni bora kuiga tabia nzuri za watu na wala sio mapungufu yao. Mwisho, watoto kutoka SU walisema kwamba, mafunzo aliyopata mhusika Mtu asiyeweza kuona, kutoka kwa ulimwengu yalifaa wengine. Awali,

### 4.2.3 Mlemavu kama Mhusika Anayenyanyapaliwa

Unyanyapaa ni hali ya kuchukia na kuepuka mtu au kitu kwa kutopendezwa na sifa na mkao wake. Awali, watu wenye ulemavu walisawiriwa kupitia dhanagande mbalimbali kwa mfano, watu wasio kamili, watakatifu, wasio na hatia, viumbe wa kuhurumiwa, tishio na hatari kwa watu wengine na wao wenyewe (Wolfensberger, 1985; Kriegel, 1987). Mijadala ya aina hii huwafanya watoto wawahurumie au hata kuwaogopa wahusika walio na ulemavu. Badala ya kupata ufahamu na kukubalika kwa watu wenye ulemavu, watoto hujifunza kile kinachowatofautisha watu walio na ulemavu na jamii pana (Blaska, 2004). Kulingana na watoto kutoka SK, SJ na SU hali hii huchangia kunyanyapaliwa kwa mhusika mtoto mwenye ulemavu. Hii ilikuwa baada ya watafitiwa

kusoma hadithi ya *Daudi Mlemavu* (Jefwa, 2000), na kisha kutoa maoni yao kuhusu namna mhusika aliye na ulemavu alivyo nyanyapaliwa na wenzake katika jamii ya msimulizi. Maoni yao yalikuwa kama yafuatavyo:

SK: Penda mwenzako hata kama ana ulemavu. SJ: Tusidharau mtu aliye na ulemavu.

SU: Tusitusi wala kudharau mtu aliye na ulemavu.

Watoto kutoka SK walieleza kuwa, ni vyema kuwapenda watu walio na ulemavu badala ya kuwanyanyapaa kama vile Daudi alivyonyanyapaliwa na wenzake kwa kuwa na maumbile tofauti. Pia, watoto kutoka SJ na SU walieleza kuwa, Daudi alidharauliwa na kunyanyapaliwa na wanafunzi wenzake ambao walimpokonya vitabu vyake. Isitoshe, walimdhalilisha kwa kumpa jina la kejeli "Daudi Mlemavu." Kunyanyapaliwa huku kulifanya Daudi kuwa mpweke kiasi kwamba, alitaka ahamishwe kutoka shule ya watoto jumuishi ya Mudete hadi shule ya watoto walio na ulemavu ya Kakamega. Licha ya kunyanyapaliwa na wenzake, Daudi hakuwaambia wazazi wake sababu kuu ya kutaka kuhama shule jumuishi. Alidai kuwa anataka kujumuika na watoto walio na ulemavu ili kujiondolea upweke kwani kujumuika nao, kungemfurahisha. Msimulizi amechora taswirawanayopitia watoto walio na ulemavu katika shule jumuishi. Aidha, watoto kutoka SU waliongeza kuwa, ni jukumu lao kujichunga wakati wanaponyanyapaliwa na jamii pana. Vilevile, walitiana moyo kwa kusema kuwa, hata ukichekwa kwa kuwa na ulemavu, haustahili kufa moyo kwani siku moja utafanikiwa maishani. Kauli za watoto kutoka SK, SJ na SU zinaingiliana na za Copenhaver (1999) na Fountas & Pinnell (2006) wanaosema kuwa, fasihi ya watoto haisaidii tu wanafunzi kukuza ujuzi wa kusoma na lugha bali pia, inaweza kubadilisha mitazamo na maoni ya wanafunzi. Ni wazi kwamba, watoto kutoka SK, SJ na SU wamethibitisha kuwa, mhusika mtoto aliye na ulemavu katika hadithi, amenyanyapaliwa kwa kurejelea mifano tofauti.

Kwa mujibu wa Schur (2002) kuna uwezekano mdogo wa watu wenye ulemavu kuolewa, uwezekano mkubwa wa kuishi peke yao, na uwezekano mdogo wa kushirikiana na marafi ki nje ya nyumba au kushiriki katika masuala ya kidini, burudani, vikundi au shughuli nyinginezo. Akisisitiza kauli hii, Schur (Keshatajwa) anaongeza kuwa, watu wenye ulemavu hunyanyapaliwa zaidi na jamii. Suala la unyanyapaa lipo katika hadithi ya Kesho! Kesho! (Hussein, 2009). Watoto kutoka SK, SJ na SU walitoa maoni yao kuhusu namna msimulizi alivyonyanyapaa mhusika aliye na ulemavu. Unyanyapaa huu umesawiriwa kupitia mhusika Mtu ambaye hawezi kuona. Watoto kutoka SK, SJ na SU walitoa maoni kwamba;

SK:Tusidharau watu wenye ulemavu.

SJ:Tusikilize wanachokisema watu wenye ulemavu.

SU:Tusiwapuuze watu walio na ulemavu.

Watoto kutoka JK, RJ na TU wanakubalina kwamba, katika hadithi ya *Kesho! Kesho!* (Hussein, 2009) mhusika mwenye ulemavu ananyanyapaliwa na jamii kupitia matendo yao. Mathalan, walieleza kuwa, katika jamii ya msimulizi, umati wa watu ulimwona mtu mwenye ulemavu kama maskini na hivyo basi, kumpuuza kipindi alichowahitaji. Ukweli ni kwamba, kauli za wanafunzi kutoka SK, SJ na SU zimeonesha kuwa, jamii ya msimulizi ina mnyanyapaa mhusika aliye na ulemavu. Aidha, wanafunzi kutoka SU walidai kuwa, si vyema kuwapuuza watu walio na ulemavu.

#### 4.2.4 Mlemavu kama Mhusika wa Kudharau

liwaKudharau ni tabia ya kukosa kuthamini mtu au kitu hasa kwa kukivunjia heshima. Kwa mujibu wa Dyches na Prater (2005) watafiti wengi wametathmini vitabu vilivyo na wahusika walio na ulemavu na kugundua kuwa, usawiri mwingi unaonesha mitazamo hasi kwa mhusika aliye na ulemavu. Kwa mfano, kulingana na maoni ya watoto wa SK, SJ na SU mhusika Daudi katika hadithi ya *Daudi Mlemavu* (Jefwa, 2000) anadharauliwa na wanafunzi wenzake mwanzoni mwa hadithi kwa sababu ya kuwa na ulemavu wa miguu. Baadhi ya kauli walizotoa ni kama vile:

SK:Tusichukue vitu vya watu ambao hawajiwezi.

Tusiwape wenzetu wenye ulemavu majina ya kejeli.

SJ:Tusipige watu walio na ulemavu.

Tusichekelee watu walio na ulemavu.

SU:Tusisukume watu walio na ulemavu.

Watu wakikuchekelea siku moja utafanikiwa

Watafitiwa kutoka SK walieleza kuwa, Daudi alipokonywa vitu vyake kwa sababu ana ulemavu. Aidha, watoto wa SK walisema kwamba, si vyema kuwapa wenzao wenye ulemavu majina ya kejeli kwani kwa kufanya hivyo, wanawavunjia heshima na hata kuwadharau. Licha ya kufahamika kama Daudi, watoto kutoka SK walidai kuwa mhusika Daudi alipewa jina la utani la 'Daudi Mlemavu' kwa kuwa, alidharauliwa na wenzake kwa kuwa na maumbile tofauti. Hata hivyo, Smith-D'Arrezo na Moore-Thomas (2010) wanaamini kwamba, fasihi hutumiwa kufunza mtu kuwa na uwezo wa kujinasibisha na hisia za mtu mwingine hasa yule anayeoonewa. Kauli hii inaungwa mkono na Roling (2013) anayeongeza kwamba, watoto wengi wanaelewa kuwa watu hunyanyaswa kwa sababu tofauti. Aidha, kwa kusoma hadithi ambayo mhusika anaonewa kutokana na ulemavu wake, msomaji anaweza kujinasibisha na hisia za mhusika huyo hasa kipindi ambacho amewai kuonewa au hata kusumbuliwa na wenzake. Aidha, watoto kutoka SJ na SU waliongeza kuwa, si vyema kucheka watu walio na ulemavu. Maoni ya watafitiwa kutoka SJ na SU yanashahabiana na yale ya McGrail na Rieger (2014) ambao wanasema kuwa, mhusika mwenye ulemavu anaweza kuwa chanzo cha kejeli. Vilevile, watoto kutoka SU walidai kuwa, katika ulimwengu halisi na hata kwenye hadithi za watoto, watoto walio na ulemavu hudharauliwa kwa kusukumwa na kuchekelewa na wengine ambao hawana ulemavu.

Mhusika Mtu asiyeweza kuona katika hadithi ya *Kesho! Kesho!* (Hussein, 2009) anadharauliwa na umati wa watu ambao unampuuza na kumwona kama mwendawazimu na hata ombaomba. Kulingana na Hodkinson (2017), katika baadhi ya hadithi, wahusika ambao hawana ulemavu hucheka na kudhihaki wahusika walio na ulemavu. Watoto kutoka SK, SJ na SU walieleza yafuatayo:

SK:Umati wa watu unamdharau mhusika mwenye ulemavu na kumwona kama mwendawazimu.

SJ:Mhusika mwenye ulemavu anapuuzwa na watu.

Mhusika mwenye ulemavu ni mwombaji.

SU:Mhusika aliye na ulemavu amedharauliwa.

Watu walitaka kumuibia kwa kuwa na ulemavu.

Watafitiwa kutoka SK, SJ na SU walibaini kwamba, licha ya umati katika jamii ya msimulizi kumsikiliza mtu asiyeweza kuona, umati ule ulimdharau mtu yule na kumuona kama mwendawazimu. Aidha, kulingana na watoto kutoka SJ, katika jamii ya msimulizi, wahusika wengine walimtazama mtu mwenye ulemavu na kumwona kama maskini kisha kuondoka. Pia, watoto kutoka SU walidai kuwa, watu katika jamii ya msimulizi walitaka kumpokonya mali yake mtu mwenye ulemavu na wala sio kumsaidia kufumbua fumbo lake. Kauli za watoto kutoka SK, SJ na SU zinaonesha kuwa, mhusika aliye na ulemavu anadharauliwa.

#### 4.2.5 Mlemavu kama Mhusika Mnyonge

Kulingana na Solis (2007) wahusika walio na muonekano tofauti wa kimwili mbali na kawaida mara nyingi huainishwa kama viumbe wanyonge. Mnyonge ni mtu asiyekuwa na nguvu. Kisa cha *Daudi Mlemavu* (Jefwa, 2000) kinapoanza, mhusika Daudi anaanza kuzungumza kwa nafsi yake. Daudi anasikitika kwamba, hawezi kucheza kama wenzake na hata kujionea huruma. Kauli hii inashahabiana na maoni ya Rubin na Watson (1987) wanaosema kuwa, adui mkubwa wa mtu mwenye ulemavu ni mlemavu mwenyewe kwa kuwa, husawiriwa kama kiumbe wa kujihurumia. Pia, watoto kutoka SK, SJ na SU waliohusishwa katika utafiti, walitoa maoni yao kuhusu mhusika mtoto aliye na ulemavu baada ya kusoma hadithi ya *Daudi Mlemavu* (Jefwa,200) na kutaja yafuatayo:

SK:Mtu anastahili kujipigania hata kama ana ulemavu.
SJ:Tujisaidie wenyewe.
Ulemavu usituzuie kusoma shule tunayotaka.
Daudi hakukataa jina la kubandikwa.
SU:Tunapaswa kujiitikia.
Tusaidie walemavu hasa wale ambao hawawezi kutembea.

Watoto kutoka SK, SJ na SU walitoa maoni yao kuhusu namna mhusika Daudi alivyodhalilishwa na wanafunzi wenzake kwa kuwa mnyonge. Watoto kutoka SK na SJ walieleza kuwa, mtu anastahili kujipigania hata kama ana ulemavu. Kulingana na watoto kutoka SK, mhusika Daudi alipokonywa vitu vyake kama vile vitabu na wanafunzi wenzake kwa kuwa, hakuwa na uwezo wa kuwakimbiza. Aidha, watoto kutoka SJ walieleza kuwa, mhusika Daudi alikuwa mnyonge kwa sababu, wanafunzi wenzake walimbandika jina la utani 'Daudi Mlemavu'. Walimpa jina hili la utani kwa kunasibisha na maumbile yake. Vilevile, watoto kutoka SJ waliongeza kuwa, Daudi ni mhusika mnyonge kwani alitaka uhamisho kutoka shule jumuishi ya Mudete hadi ile ya watoto walio na ulemavu ya Kakamega kwani, alitaka awe na watoto wenzake walio na ulemavu. Hata hivyo, kulingana na watoto kutoka SU, ingawa mhusika Daudi ni mnyonge kama walivyo wao, anastahili kujikubali. Maoni ya watoto kutoka SU ni kuwa, kabla ya kumnasa mwizi, Daudi alijiona mtu mnyonge ambaye hawezi kuchangia chochote katika jamii.

Pia, hadithi ya *Kesho! Kesho!* (Hussein, 2009) msimulizi amemsawiri mhusika mtoto aliye na ulemavu kama mhusika mnyonge. Aidha, watoto kutoka SK, SJ na SU walithibitisha hili kupitia kauli zao. Kwa mfano, watafitiwa walieleza kuwa:
SK:Mtu mwenye ulemavu hawezi kutembea bila mkongojo.
Tusaidie watu walio na ulemavu.
SJ:Watu wenye ulemavu huhitaji msaada.
Baadhi ya watu wenye ulemavu huhitaji miwani au mikongojo.
SU:Tusaidie watu walio na ulemavu.
Watu wasioona wanahitaji mkongonjo.

Kwa mujibu wa watoto kutoka SK, SJ na SU mhusika ambaye hawezi kuona katika hadithi ya *Kesho! Kesho!* (Hussein, 2009), hawezi kutembea bila ya mkongojo wake na hivyo basi, ni mnyonge na huhitaji usaidizi. Waidha, watoto kutoka SJ walisema kuwa, mhusika Kalpan pamoja na wazazi wake hawawezi kufanya chochote bila miwani ya kuonea. Pia, watoto kutoka SU walishadidia maoni ya wenzao kwa kuongeza kuwa, watu wasioona hawawezi kutembea bila mikongojo au hata kusaidiwa na hivyo basi, ni wanyonge. Kauli za watoto kutoka SK, SJ na SU zinaingiliana na mawazo ya Kristanti (2016) ambaye anasema kuwa, mara nyingi, watu walio na ulemavu huchukuliwa kama binadamu wasio na uwezo wa kufanya kazi zinazofanywa na watu ambao hawana ulemavu. Hata hivyo, ni dhahiri kwamba, licha ya ulemavu, watu wenye ulemavu wanaweza kufanya kazi zinazofanywa na watu ambao hawana ulemavu. Mathalan, Zoltán (2023) anaongeza kuwa, watu wanaoishi na ulemavu wanaweza kuzidi uwezo wa wale wanaoachukuliwa kuwa wazima.

Vilevile, maoni ya watoto kutoka SK, SJ na SU yanaingiliana na mhimili wa nadharia ya Udenguzi yake Derrida (1976) unaosema kuwa, hakuna kazi ya mwisho ya kifasihi na fasiri mbalimbali zinaweza kutolewa na wahakiki tofauti kuhusu jambo moja ambalo linaweza kukinzana maadamu kuna ushahidi wa kutosha. Ni wazi kwamba, watoto kutoka SK, SJ na SU wametoa fasiri mbalimbali kumhusu mtoto aliye na ulemavu kama vile; shujaa, mnyonge, wa kuigwa, wa kudharauliwa, mwenye uwezo, anayenyanyapaliwa na hata wa kudharauliwa.

## 5.0 Hitimisho

Makala hii imebainisha namna watoto wasomaji wa gredi ya kwanza na ya pili wanavyofasiri mhusika mtoto aliye na ulemavu kwa kuchanganua hadithi teule. Kwa mfano, watoto wa gredi ya kwanza walimfasiri mhusika aliye na ulemavu kama mwenye kuendeleza ushirikiano na mapenzi, mwenye kuonewa huruma/ kudunishwa na hata kama anayebaguliwa. Aidha, watoto wasomaji wa gredi ya pili walimfasiri mhusika aliye na ulemavu kama shujaa, wa kuigwa, wa kunyanyapaliwa, wa kudharauliwa na hata mnyonge.

## Maelezo ya Ufupisho

**NCPWD:** *The National Council for Persons with Disabilities in Kenya:* Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu Nchini Kenya.

**SK** - Shule ya Kawaida, **SJ** - Shule Jumuishi na **SU**- Shule ya watoto walio na ulemavu.

## MAREJELEO


Ali, A. (2019). Kuchunguza Dhamira ya Mapenzi katika Riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena* ya Said Mohamed. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. (Haijachap ishwa).

Ayala, E. C. (1999). “Poor little things” and “Brave little souls”: The portrayal of individuals with disabilities in children's literature. In, *Literacy Research and Instruction,* 39 (1). Kur. 103-117.

Aylestock, N. (2009). *Supreme Heroes.* S.I.: Iuniverse Inc.

Azano, A. P., Tackett, M., & Sigmon, M. (2017). Understanding the puzzle behind the pictures: A content analysis of children’s picture books about autism. *AERA Open, 3*(2). Kur. 1–12. https://doi.org/10.1177/2332858417701682

BAKIZA (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha.* Nairobi: Oxford University Press.

Bakize, L. H. (2014). *Utangulizi wa Fasihi ya Watoto.* Dar es Salaam: Moccony Printing press.

Beckett, A., Ellison, N., Barrett, S., & Shah, S. (2010). ‘Away with the fairies?’*Disability within* primary-*age children's literature. In, Disability & Society, 25*(3). Kur. 373-386.

Cameron, C., & Moore, M. (2014). Disability studies. In, *Disability studies: A student’s guide.* Kur. 37-39.

Crow, L. (1990). Disability in children's litera ture. In, *Transcript of a seminar given to the Arts Council Literature Department. Available online at: http://www. roaringgirl. com/work/ disability-in-childrens-literature* (acessessed 26 November, 2024).

Copenhaver, J. F. (1999) ‘The intersections of response and ethnicity: elementary school students respond to multicultural children’s literature’ [online at http://files.eric.ed.gov/full text/ED436780.pdf]. Retrived on 02/01/2025.

Derrida, J. (1976). *Of Grammatology.* Balti more: Johns Hopkins University Press.

Dulin-Keita, A., Hannon Iii, L., Fernandez, J. R., & Cockerham, W. C. (2011). The defining moment: Children's conceptualization of race and experiences with racial discrimination. In, *Ethnic and racial studies,* 34(4). Kur. 662-682.

Dyches, T. T., & Prater, M. A. (2005). Charac terization of developmental disability in children's fiction. In, *Education and Training in Developmental Disabilities.* Kur. 202-216.

Fountas, I. & Pinnell, G. S. (2006). *Teaching for Comprehending and Fluency: thinking, talking, and writing about reading, K-8.* Ports mouth, NH: Heinemann.

Howard, M. (1999). "Social exclusion zone". *Guardian Society* [online] 10 September. [Accessed September 2022] Hussein, A. (2009). *Kesho! Kesho!* Nairobi: O.U.P.

Jefwa, J. (2000). *Daudi Mlemavu.* Nairobi: EAEP.

Kombo, D. K. and Tromp, L. A. (2006). *Propos sal and Thesis Writing: An Introduction.* Nairo bi: Paulines Publications.

Kriegel, L. (1987). The cripple in literature. *Images of the disabled, disabling images*. Kur. 31-46.

Kristanti, F. (2016). Dignifying children through inclusive children’s literature. *Journal of Language and Literature,* 16(01). Kur. 63-69.

Leininger, M., Dyches, T. T., Prater, M. A., & Heath, M. A. (2010). Newbery award winning books 1975-2009: How do they portray disabil ities? *Education and Training in Autism and Developmental Disabilities*, 583-596.

Levinson, S., & Mailloux, S. (1988). *Interpret ing law and literature: A hermeneutic reader.* Northwestern University Press.

Lidubwi, J. N. (2017). Representation of disability in Media: A study of abled differently program. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Macharia, F. N. (2021). Tathmini ya Hadithi Fupi zilizowasilishwa katika *British Broadcast ing Corporation:* Mtazamo wa Edgar Allan Poe na Leech (1969). Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Mahenge, E. G. (2017). Msigano wa Majina ya Walemavu katika Jamii ya Wazungumzaji Kiswahili: Mfano kutoka Tanzania. *Kioo cha Lugha,* 11(1). Kur. 78-87. UDSM.

Maina, D. (2022). *Tupendane Sote.* Nairobi: Spotlight Publishers.

McGrail, E., & Rieger, A. (2014). Humor in literature about children with disability: What are we seeing in literature? In, *The Educational Forum,* 78(3). Kur. 291-304.

Mpemba, T. (2015). Kufasiri, Kukalimani na Kurudufu Matini kwa Lugha Nyingine: Tulikotoka hadi Tulipo Sasa. *Kioo cha Lugha,* 13(1). Kur. 81- 102.

Mutugu, B. N. (2019). Taswira za Ulemavu kama Mtindo katika Riwaya Teule za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi. Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Mwanzu, D. M. (2021). Mshabaha na tofauti Kati ya Hadithi ya Kisasa na Ngano. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Ngugi, P. M. (2013). afsiri katika fasihi ya watoto: Mbinu na mikakati. Katika S. Omari & G. Mrikaria (Wahariri), *Mulika Journal,* 32. Kur. 12–26.

The National Council for Persons with Disabilities (2003). *Persons with Disabilities Act, 2003.* Nairobi: Government Printers.

Omoga, R. G. (2018). Mwananchi wa Kawaida kama Mdhulumu wa Maslahi yake katika Tamthilia za *Kilio cha Haki, Amezidi na Mstahiki Meya.* Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Pirsl, D., & Popovska, S. (2013). Media mediated disability: How to avoid stereo otypes. *International Journal of Scientific Engineering and Research (IJSER),* 1(4). Kur. 42-45.

Rajula, T. (2019). *Rafiki yangu Kilomi.* Nairobi: no Boundaries Ltd.

Republic of Kenya. (2006). *Sexual Offense Act,* 2006. Nairobi: Government Printers.

Republic of Kenya. (2010). *The Constitution.* Nairobi: Government Printers.

Roling, K. (2013). Portrayal of Characters with Disabilities within K-6 Fictional Litera ture. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Northern Lowa. (Haijachapishwa).

Rubin, E., & Watson, E. S. (1987). Disability bias in children's literature. In, *The Lion and the Unicorn, 11(1).* Kur. 60-67.

Schur, L. (2002). The difference a job makes: The effects of employment among people with disabilities. *Journal of Economic Issues, 36(2).* Kur. 339-347.

Shirika la Kazi Duniani. (2007). *Kazi za Ndani Zenye Madhara kwa Watoto: Kijitabu cha Maelezo Mafupi.* Geneva: IPEC. Shirika la Kazi Duniani. (2007). *Kufanikisha Fursa Sawa za Ajira kwa Watu wenye Ulemavu kupitia Sheria: Mwongozo,* Dar es Salaam.

Sikirivwa, M. K. (2015). Deconstruction theory and its background. In, *Journal of English Literature and Culture, 3*(7). Kur. 44-47.

Smith-D'Arezzo, W. M., & Moore-Thomas, C. (2010). Children's Perceptions of Peers with Disabilities. In, *Teaching exceptional children plus, 6*(3). Kur. 3.

Solis, S. (2007). Snow White and the seven "dwarfs" Queercripped. In, *Hypatia,* 22(1). Kur. 114-131.

Sumara, D. J. (2002). *Why reading literature in school still matters: Imagination, interpretation, insight.* Routledge.

Tanjung, P. (2020). Series of Discrimination among Children. In, *Kata Kita: Journal of Language, Literature, and Teaching, 8*(2). Kur. 135-143.

Taylor, P. A. (2014). Meaning, expression, and the interpretation of Literature. In, *The Journal of Aesthetics and Art Criticism, 72*(4). Kur. 379-391.

United Nations Children's Fund 2013 United Nations Children's Fund The state of the world's children 2013: Children with disabilities 2013: Children with disabilities. UNICEF (2013) https://www.unicef.org/media/84886/file/SOWC-2013.pdf

United Nations. (2022, February 17). *Utafiti na ushahidi juu ya watoto wenye ulemavu:* UNICEF. Habari za UN. https:news.un.org/sw/story/2022/02/1137782

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wolfensberger, W. (1985). Social role valorization: A new insight, and a new - term, for normalization. *Australian Association for the Mentally Retarded Journal,* 9(1), 4-11.

Zhang, C., & Morrison, J. W. (2010). Imparting cultural values to Chinese children through literature. In, *International Journal of Early Childhood,* 42. Kur. 7-26.

Zoltán, Á. (2023). The situation and sports opportunities of people with disabilities. *Bulletin of Medical Sciences, 96*(1). Kur. 51-58. https://www.vocabulary.com. Retrieved on 1st February, 2025.